



JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
TUME YA TAIFA YA UCHAGUZI



TAARIFA KWA UMMA KUHUSU UCHAGUZI MDOGO WA MADIWANI
KATIKA KATA SITA (06)

Dodoma, 28 Oktoba, 2021

Tume ya Taifa ya Uchaguzi imepokea barua kutoka kwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais (TAMISEMI), yenye Kumb. Na. CCB.126/443/01/73 ya tarehe 26 Oktoba, 2021, ikitoa ridhaa ya kujaza nafasi wazi za Udiwani katika mamlaka za Serikali za Mitaa. Kata zenye nafasi wazi za Udiwani ni: Bomalang'ombe (Halmashauri ya Wilaya ya Kilolo), Nyabulanda (Halmashauri ya Wilaya ya Nyang'wale), Ipwani (Halmashauri ya Wilaya ya Mbarali), Likombe (Halmashauri ya Manispaa ya Mtwara), Handali (Halmashauri ya Wilaya ya Chamwino), na Nalasi Mashariki (Halmashauri ya Wilaya ya Tunduru). Nafasi hizo wazi zimetokana na sababu mbalimbali zikiwemo vifo na kujiuzulu.


Kwa kuzingatia masharti ya Kifungu cha 13 (3) cha Sheria ya Uchaguzi ya Serikali za Mitaa, Sura ya 292, Tume imeandaa chaguzi ndogo ili kujaza nafasi wazi za Udiwani kwenye kata hizo sita (06). Ratiba ya chaguzi hizo ndogo ni kama ifuatavyo:-

NA.	TUKIO	TAREHE
1.	Wagombea kuchukua Fomu za Uteuzi	09 - 15 Novemba, 2021
2.	Uteuzi wa Wagombea	15 Novemba, 2021
3.	Kampani za Uchaguzi	16 Novemba hadi 10 Desemba, 2021
4.	Siku ya kupiga kura	11 Desemba, 2021

Tume ya Taifa ya Uchaguzi tayari imevitaarifu Vyama vya Siasa na inavikumbusha Vyama hivyo pamoja na wadau wote wa Uchaguzi kuzingatia Sheria, Kanuni, Maadili

ya Uchaguzi, Taratibu, Miongozo na maelekezo yatakayotolewa na Tume katika kipindi chote cha Uchaguzi mdogo.

Imetolewa na:



Gerald G.J. Mwanilwa
Kaimu Mkurugenzi wa Uchaguzi
TUME YA TAIFA YA UCHAGUZI